



WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

ISSN: OOOOO401 | Toleo Na. 03 | Mei - Oktoba, 2022



BRELA
NA URASIMISHAJI BIASHARA

YALIYOMO

3

BRELA, FCC WASAINI MAKUBALIANO



4

KAMPUNI ZINAZODAIWA ZISIFUTWE- DKT. KIJAJI



9

BRELA, BPRA ZATAKИWA KUANDAA
MKAKATI WA KULINDA KAZI ZA WABUNIFU



BODI YA UHARIRI

wajumbe

Tawi Kilumile

Theresa Chilambo

Abdulrahman Songoro

Neema Kitala

Nehemia Mihayo

Alpha Nuhu

Roida Andusamile

Katibu

Andrew Mkapa
Mwenyekiti

BRELA, FCC wasaini makubaliano



Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa (aliyeketi kulia) akitia saini makubaliano ya ushirikiano na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani (FCC) Bw. William Erio (aliyeketi kushoto), ili kurahisisha mazingira ya uwekezaji nchini.

Na Njwaba Mwaijibe

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imesaini makubaliano ya ushirikiano na Tume ya ushindani (FCC), wakati huo huo FCC ikisaini na Shirika la kuhudumia viwanda vidogo (SIDO), yenye lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

Akizungumza mara baada ya utiaji saini makubaliano ya ushirikiano huo hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Afisa Mtendaji Mkoo wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa alisema BRELA ipo tayari kutoa ushirikiano kwa Taasisi hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa mbalimbali pale zinapohitajika.

Bw. Nyaisa alisema kuwa ushirikiano wa taasisi hizo za Serikali ambazo zinawezesha biashara utatoa fursa kwa wawekezaji kupata masoko ya

uhakika huku bidhaa zao zikiwa zinatambulika na mamlaka husika.

"Ndugu wanahabari tunaomba muufahamishe Umma wa watanzania na wawekezaji kuwa utiaji saini huu unalenga kufungua milango zaidi ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuondoa migongano ya hapa na pale ambayo inaweza kuchelewesha michakato ya urasimishaji wa biashara, hivyo tunafanya haya kuhakikisha wawekezaji wanakamilisha michakato ya ufanyaji biashara kwa wakati," alifafanua Bw. Nyaisa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkoo wa FCC, Bw. William Erio alisema yanapotokea malalamiko ya mtu kutumia alama ya biashara ya mwine, FCC huomba taarifa kutoka BRELA kwani ndio yenye dhamana

ya kusajili majina ya biashara, kampuni na alama za biashara.

Wakati huo huo Mkurugenzi Mkoo wa SIDO, Profesa Sylvester Mpanduji alisema SIDO kama mlezi wa viwanda vidogo itahakikisha inatoa ushauri na kuhimiza wadau wanaopata mafunzo kurasimisha biashara zao BRELA, ili kukidhi vigezo katika soko la ndani na nje ya nchi.

Utiaji saini makubaliano hayo yamefanyika tarehe 23 Juni, 2022 katika ofisi za FCC, Jijini Dar es Salaam, ikiwa ni muendelezo wa utekelezaji wa maagizo ya Waziri mwenye dhamana ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, yanayozitaka Taasisi chini ya Wizara hiyo, kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuvutia wawekezaji na kufanya Tanzania kuendelea kuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji.

Kampuni zinazodaiwa zisifutwe- Dkt. Kijaji

Na Mwandishi wetu

WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) ametoa agizo kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kutozifunga kampuni zinazodaiwa badala yake kukaa na Wafanyabiashara na kutatua changamoto walizonazo katika masuala ya Leseni na Usajili wa Makampuni ili kuboresha Mazingira ya Biashara.

Waziri Dkt. Kijaji alitoa agizo hilo jijini Dodoma, wakati wa kikao cha Kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilipopokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya BRELA.

Alieleza kuwa Serikali imeendelea kutengeneza Mazingira ya Biashara kuitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara BLUEPRINT hivyo ameitaka BRELA kuendelea kutoa elimu ya Usajili wa Makampuni, Leseni na Umiliki Manufaa.

Wajumbe wa Kamati hiyo walitoa maoni na mapendekezo mbalimbali yanayolenga kuboresha huduma za BRELA ikiwemo Uwasilishaji wa taarifa za wamiliki manufaa, uhusiano wa biashara katи ya Tanzania Bara na Zanzibar na Sheria ya Leseni za Biashara na usajili wa viwanda ya mwaka 1967 ambayo inauhitaji mkubwa wa kuifanya marekebisho.

Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Mhe. David Kihenzile (Mb) alipongeza BRELA kwa kazi nzuri na kusema kuwa ni wakati sasa wa Wizara kuzileta pamoja taasisi zake za BRELA, EPZA na TIC ambazo



Dkt. Ashatu Kijaji (Mb)

zinahusika na utoaji wa Leseni au vibali ili kuwa na takwimu sahihi za Wafanyabiashara Nchini nzi nzima.

Akijibu baadhi ya maswali ya Wajumbe wa Kamati hiyo Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa ameahidi kuwa BRELA itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utoaji wa huduma na kutumia mifumo ya Kielektroniki ya Utoaji Huduma za Sajili (ORS) na Utoaji wa Leseni za Biashara (NBP).

Awali akiwasilisha taarifa ya usajili wa Makampuni pamoja na jukumu la utoaji Leseni Kaimu Mkuu wa sehemu ya Makampuni BRELA Bi. Leticia Zavu alisema kuwa BRELA imekuwa ikitoa elimu ya mara kwa mara kuitia vyombo mbalimbali vya habari kwa waliosajili kampuni, kampeni juu ya matumizi ya mifumo ya TEHAMA na ukaguzi elimishi kwa kuwatemeblea Wafanyabiashara kuwasikiliza na kutatua changamoto zao

BRELA, TAKUKURU kushirikiana



Afisa Mtendaji Mkoo wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa (wa pili kulia walioketi), Mkurugenzi Msaidizi wa Operesheni kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Bw. Saimon Maembe (aliyeketi katikati), wakiwa katika picha ya pamoja na Washiriki wa kikao kazi baina ya taasisi hizo, tarehe 8 Julai, 2022.

Na Theresa Chilambo

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), zimekusudia kuwa na mashirikiano ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Serikali.

Katika kufanikisha hilo, taasisi hizo zimekutana katika kikao kazi cha siku mbili kilichofanyika katika Ukumbi wa Mkutano Nashera hoteli, mkoani Morogoro kujadili maeneo ya muhimu ya ushirikiano na changamoto zinazojitokeza wakati wa kutekeleza majukumu.

Afisa Mtendaji Mkoo wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, alieleza kuwa Mkutano kat i ya taasisi hizo utaleta maboresho makubwa ya kiutendaji kwa pande zote mbili.

"Tukiwa kama Wakala anayehusika katika kukuza uchumi kwa kurasimisha biashara, viwanda na uwekezaji nchini, tunajukumu la kuzingatia kuwa Sajili za kila aina zinafanyika kihalali na zinazingatia taratibu zote zilizowekwa kwa mujibu wa sheria katika kuhalalisha biashara.

Ni matarajio yangu kwamba kikao hiki kitakwenda kuleta mabadiliko katika Taasisi zetu hususan kwenye changamoto mbalimbali tunazopipata ili kuleta ufumbuzi wa pamoja kwa manufaa ya Taasisi hizo mbili," alisema Bw. Nyaisa.

Alibainisha kuwa kikao kazi hicho kitapitisha

Rasimu ya Makubaliano [Memorandum of Understanding [MOU] baina ya BRELA na TAKUKURU yenye dhamira ya kuleta umoja na mshikamano kwa Taasisi hizo katika kutimiza majukumu ya kila siku.

Akimuwakilisha Mkurugenzi Mkoo wa TAKUKURU, Mkurugenzi Msaidizi wa Operesheni, Bw. Saimon Maembe, alisema kuwa kikao hicho ni muarobani wa changamoto sugu wanazokutana nazo katika utendaji kazi.

Bw. Maembe alifafanua kuwa taasisi hizo mbili zinafanya kazi kwa karibu sana hasa kwa kuwa taarifa zote kuhusu Makampuni zinapatikana BRELA na kuongeza kuwa, mara nyingi TAKUKURU imekuwa ikihitaji taarifa mbalimbali au ufanuzi kuhusu taarifa za makampuni.

Kikao kazi hicho pamoja na mambo mengine, kililenga kutengeneza mfumo mzuri wa kubadilishana taarifa, hasa kwa kuzingatia kuwa BRELA imeboresha upatikanaji wa taarifa kwa kuwa huduma zake zote zinapatikana kwa njia ya mtandao.

Kikao hicho kilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 30 ambao ni Makamanda wa Kanda zote za Dar es Salaam, Wakurugezi wa Uchunguzi na Maafisa uchunguzi kutoka Dar es Salaam na Makao Makuu Dodoma pamoja na Maafisa Usajili kutoka BRELA.

WIPO yapongezwa kuendeleza ubunifu

Na Roida Andusamile

AFISA Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa amepongeza Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO) kwa jitihada inazozifanya za kuendeleza kazi za ubunifu kwa maendeleo ya nchi wanachama.


Pongezi hizo alizitoa wakati akiwasilisha taarifa ya nchi kuhusu Miliki Ubunifu na ushirikiano katika Tanzania na WIPO katika Mkutano Mkuu wa 63 wa Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO), uliofanyika Geneva Uswisi.

Bw. Nyaisa alisemajitihada hizo za kuendeleza kazi za ubunifu kwa maendeleo ya nchi wanachama, zitazaar.

matunda na kuendeleza bunifu mbambali na kuleta tija kwa nchi wanachama.

Alieleza pia ushirikiano kati ya Tanzania na WIPO utalenga katika kusaidia wajasiriamali na vijana katika kutumia Miliki Ubunifu kwa maendeleo ya ubunifu.

Mkutano huo wa siku saba ulioanza tarehe 14 Julai, 2022, ulihudhuriwa pia na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Bishara na Mali, (BPRA) Zanzibar, Bi. Mariam Mliwa Jecha, Mkuu wa Idara ya Uraghbishi wa Ushindani kutoka Tume ya Ushindani (FCC) Bi. Magdalena Utouh pamoja na Msajili Msaidizi Mkuu kutoka BRELA, Bi. Loy Mhando.



AFISA Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa akiwasilisha taarifa ya nchi kuhusu Miliki Ubunifu na ushirikiano katika Tanzania na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO) katika Mkutano Mkuu wa 63 wa WIPO, uliofanyika Geneva Uswisi.

Taasisi zakutana kuboresha huduma za uwekezaji



Washiriki wa Mkutano wa Taasisi zinazounda huduma ya pamoja wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa kikao kilichofanyika mjini Morogoro hivi karibuni.

Na Mwandishi wetu,

WAKALA wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA) yaungana na taasisi zinazounda huduma ya pamoja ili kuendelea kujadili mikakati ya uboreshaji wa huduma kwa wawekezaji nchini katika kikao kilichofanyika ukumbi wa Mahakama Kuu mjini Morogoro na kikao kuratibiwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa, alisema majadiliano yamelenga juu ya namna bora ya kufanya maboresho ya Mfumo wa huduma kwa wawekezaji kuititia dirisha la mahala pamoja "One Stop Facilitation Center".

"Kukamilika kwa maboresho ya Mfumo wa Uwekezaji unaohusisha Taasisi mbalimbali zinazosimamia sekta ya uwekezaji hapa nchini, kutachagiza ukuaji wa sekta hiyo". alisema Bw. Nyaisa.

Aliongeza kwa kusema kuwa, matarajio ya kutumia kukuza uchumi pamoja na kupunguza mizunguko ya mchakato wa ukusanyaji wa taarifa za mwekezaji, ili kukabiliana na hali ya wawekezaji kuomba nafasi ya kuwekeza kwenye mataifa mengine ya jirani.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma kwa Wawekezaji kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Bw. John Mnali alisema, kukutana kwa Taasisi zinazohusika na utoaji vibali mbalimbali kwa wawekezaji ikiwemo sekta ya ardhi kutarahisha kupunguza malalamiko ya ucheleweshaji wa vibali hivyo, ambapo kwasasa zoezi zima litafanyika kwa njia ya mtandao, lengo ni mchakato wa uratibu wa taarifa kukamilika kwa siku moja.

"Mwanzioni ilikuwa ikiwachukuwa wawekezaji

mpaka siku saba au hata na zaidi kupata vibali hivyo lakini sasa kuna mabadiliko makubwa na lengo letu ni Mwekezaji aweze kupata vibali vyote kwa siku moja kama atakuwa amekamilisha nyaraka zote zinazohitajika", alisema Bw. Mnali.

Kikao hicho cha majadiliano ya kuboresha mfumo wa uwekezaji ni mwendelezo wa vikao vyaa kuimarisha sekta ya uwekezaji nchini na kimehusisha Wakala wa Taasisi mbalimbali kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Idara ya Uhamiaji Tanzania, Wizara ya Ardhi, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), pamoja na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC).

Sheria ya Leseni za Biashara kuboreshwa

Na Christina Njovu

WADAU wa biashara kutoka Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi wakutana na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kutoa maoni juu ya marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara Sura 208.

Hatua hiyo inafuatia mpango wa Serikali wa kuifanya marekebisho Sheria ya Leseni za Biashara Sura 208 ili iendane na hali ya sasa, baada ya kubainika kuwa Sheria hiyo imepitwa na wakati.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa Leseni kutoka BRELA, Bw. Andrew Mkapa wakati wa kikao cha kukusanya maoni ya wadau Jijini Dar es Salaam kuhusu marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara Sura 208. Bw. Mkapa amesema Sheria ya Leseni za Biashara kama ilivyo kwa sheria nyingine za nchi, haitakiwi kuwa mgando na zinatakiwa kwenda na wakati, hivyo Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, kuititia BRELA imeona ni vema kuifanya marekebisho sheria hiyo.

Bw. Mkapa ambaye alifungua kikao hicho kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA alisema, hivi sasa limeibuka suala la biashara za mitandaoni ambalo nalo linatakiwa kuangaliwa kisheria ili kwenda sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

“Hatua iliyopo sasa ni ya kikosi kazi kuchukua maoni na kuyapeleka serikalini kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho kwa sheria hiyo”, alifafanua Bw. Mkapa.



Mkurugenzi wa Leseni wa BRELA , Bw. Andrew Mkapa akifafanua jambo wakati wa kikao cha kukusanya maoni ya wadau kuhusu marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara Sura 208, Jijini Dar es Salaam.

BRELA, BPRA zatakiwa kuandaa mkakati wa kulinda kazi za wabunifu

Na Christina Njovu

MAKAMU wa Kwanza wa Rais-Zanzibar Mhe. Othman Masoud Othman ametoa Wito kwa Wizara zinazosimamia masuala ya ubunifu pamoja na taasisi zikiwemo Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) ya Zanzibar, kuhakikisha kuwa zinaandaa mikakati maalumu ya kulinda kazi mbalimbali za wabunifu.

Mhe. Othman alitoa agizo hilo hivi karibuni wakati wa ufunguzi wa Wiki ya Kitaifa ya Ubunifu

(MAKISATU) ilioambatana na maonesho ya Wabunifu, katika uwanja wa Jamhuri, Jijini Dodoma.

Alisema kuwa, nchi mbalimbali zimepata maendeleo makubwa kwasababu ya kuwa na mikakati madhubuti ya kulinda kazi za wabunifu, kwa hivyo ni vema kuwasaidia wabunifu na lazima kuwa na mikakati ya kuwasaidia, kujua ni namna gani na hatua gani za kulinda kazi hizo.

"Siku hizi vitu vingi vinafanyika kwa udanganyifu na ujanja mkubwa umekuwa ni wa kuchukua kazi za wengine, hivyo tunapaswa kuwa na mikakati

ya kulinda kazi za wabunifu", alifafanua Mhe. Othman.

Mhe. Othman aliongeza kuwa, kazi za ubunifu zisipolindwa zitakuwa hazina maana, na hii itawafanya wavuje jasho lakini bila kuwa na tija inayotokana na jasho lao, hivyo kuna haja ya kutilia mkazo suala hili kwa kuweka mikakati madhubuti.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Miliki Ubunifu Bw. Seka Kasera alieleza kuwa, kama kaulimbiu inavyosema, "Ubunifu kwa Maendeleo Endelevu," aliwataka wabunifu waliosajiliwa kuendeleza bunifu zao kwa kuziboresha kulingana na mahitaji ya jamii.

"Katika maonesho haya nimetembelea mabanda ya wabunifu na kuziona bunifu nyingi ambazo zinahitaji kuendelezwa kwa kuziboresha zaidi badala ya kuziacha kama ziliyyo," alifafanua Bw. Kasera.

Akirejea kauli ya Mgeni rasmi kuwa tangu mwaka 2019 China ndio nchi inayoongoza kwa kutoa bunifu nyingi na inaongoza kwa kutoa bunifu endelevu kwakuwa wamekuwa wakiziongezea ubora mara kwa mara kulingana na mahitaji ya jamii.

Bw. Kasera aliwashauri wabunifu ambao bunifu zao bado hazijapata ulinzi lakini zina sifa ya kupata ulinzi, kuwasiliana na BRELA kwa ajili ya kupata ulinzi juu ya uvumbuzi waliofanya.

BRELA imekuwa ikitoa elimu ya namna ya kuboresha bunifu zile ambazo zimesajiliwa na kuziendezea na kuangalia jinsi ya kushirikiana na taasisi nyingine za kikanda na kimataifa kuwasaidia kuzipatia masoko.



Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibar Mhe. Othman Masoud Othman akifungua Maonesho ya Wiki ya Ubunifu katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Maafisa Biashara watakiwa kuibua wafanyabiashara na kuwasimamia



Maafisa Biashara kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani wakisikiliza kwa makini mafunzo juu ya Sheria ya Leseni za Biashara iliyofanyika Mkoani Pwani.

Na Sheila Mfunami

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imewataka Maafisa Biashara kutoka mikoa minne ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani kuzingatia sheria za utoaji wa Leseni za Biashara katika Halmashauri zao ili waweze kuwarahisishia wafanyabiashara kupata manufaa kutoekana na jitihada zao.

Rai hiyo ilitolewa hivi karibuni na Mkuu wa sehemu ya Leseni za Biashara kutoka Idara ya Leseni (BRELA), Bw. Tawi Kilumile katika warsha ya kuwajengea uwezo maafisa biashara iliyofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Wakunga na Wauguzi (TNMC), mkoani Pwani.

Bw. Tawi alisema kuwa Maafisa Biashara wengi hawajui taratibu

za kufuata katika kutoa Leseni za Biashara kwa wafanyabishara hiyo imepelekea wengi kufanya makosa wakati wa utoaji wa Leseni.

Alibainisha kuwa Sheria ya Leseni za Biashara itawawezesha wawekezaji kufahamu taratibu zipi za kufuata na kuzingatia wanapohitaji Leseni za Biashara na BRELA imekusudia kutoa elimu juu ya taratibu za utoaji wa Leseni kwa Maafisa Biashara wote nchini.

“Lengo kuu la warsha hii ni kuwajengea uwezo Maafisa Biashara ili wajue umuhimu wa kuzingatia kanuni na sheria za utoaji wa Leseni za biashara,” alisema Bw. Tawi.

Baadhi ya Maafisa Biashara kutoka mikoa minne ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani

walifurahishwa na muitikio chanya wa BRELA katika kusikiliza changamoto zao na kuiomba BRELA kuandaa mikutano kama hii mara kwa mara ili kuimarisha uhusiano na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku kwa pande zote mbili.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wa Warsha hiyo, Afisa Biashara kutoka Manispaa ya Mtwara -Mikindani, Bi. Janeth Julius Mhegelle alisema amejifunza mambo mengi kuititia BRELA na atazingatia kanuni, taratibu na Sheria kwenye utoaji wa leseni ili kuwavutia wawekezaji na Wafanyabiashara katika kukuza uchumi wa nchi.

Mafunzo ya Sheria ya Leseni za Biashara yalianza Juni 27, 2022 hadi Julai 1, 2022.

Mchango wa BRELA katika kukuza biashara



Afisa TEHAMA wa BRELA, Bw. Hilary Mwenda (kulia) akitoa usaidizi wa usajili jina la biashara kwa mjasiriamali katika moja ya maonesho ambayo BRELA ilishiriki.

Na Nehemia Mihayo

Aristoteli aliyejikuwa mwanafalsafa muhimu wa Ugoriki aliwahi kunikuliwa akisema siri ya mafanikio katika biashara ni pale ambapo utafahamu kitu kuhusu biashara unayofanya ambacho wengine hawakijui.

Mpaka mwaka 2017 biashara ndogo na za kati zilikadiriwa kuwa zaidi ya milioni tatu ambazo nusu kati yake zilikua zikimilikiwa na Wanawake na zinachangia asilimia 27% ya jumla ya pato la Taifa (GDP).

Takwimu zinaonesha kwamba hadi kufikia mwaka 2021, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imesajili jumla ya Makampuni 12,583, Majina ya biashara 23,780, Alama za Biashara na Huduma 3,555 na Hatazo.

Pia imetua Vyeti vya Usajili wa Viwanda vyenye mtaji wa chini ya milioni mia moja 117 na Leseni kwa viwanda vyenye mtaji wa zaidi ya milioni moja 132,621 pamoja na Leseni za biashara Kundi "A" 34.

Biashara hufananishwa na maisha ya binadamu, huzaliwa, huishi na pia hufa kutokana na changamoto mbalimbali ambazo biashara husika imepitia na hivyo kushindwa kuendelea kuishi au kibiashara ni kukua.

Baadhi ya changamoto zinakua ni kutokana na

kuwa na mitaji midogo, ushindani wa kibiashara, kushindwa kujitangaza katika masoko, kukosa elimu ya urasimishaji wa biashara, migogoro baina ya wamiliki, na changamoto nyininge nydingi zinazofanana na hizo.

BRELA inamchangoo mkubwa katika kusimamia na kuhakikisha biashara ndogo na za kati zinakua kwa kuzipa usimamizi na kuzilea biashara hizo.

Katika kutekeleza hilo BRELA imeweka mikakati mbalimbali pamoja na jitihada shirikishi kuhakikisha kila biashara ambayo inasajiliwa inaendelea kukua kila siku tangu kurasimishwa kwake.

Dira ya Wakala ni kuwa taasisi ya mfano kikanda katika utoaji wa huduma bora za usajili na utoaji wa leseni za biashara. Dhima yake ni Kuweka mazingira wezeshi ya biashara nchini kwa kurasimisha biashara na kulinda miliki-ubunifu kupitia usajili, utoaji wa leseni na udhibiti wa mwenendo wa biashara.

Dira na dhima za Wakala ni dhamira halisi ya kuhakikisha kwamba taasisi inakuwa ni nguzo ya kuzishikilia biashara ambazo Wafanyakishaa na Wafanyakishaa wanazanzisha ziendelee kusimama na sio kuanguka. Zifuatazo ni baadhi ya jitihada zilizofanywa na taasisi katika kuhakikisha biashara ndogo na za kati zinakua.

UTATUZI WA MIGOGORO

BRELA imekuwa na utaratibu wa kutatua migogoro ya baina ya Wamiliki wa biashara ambao wamerasimisha biashara zao kwa mujibu wa sheria.

Migogoro hiyo mingi imekuwa ikidhoofisha ukuaji wa biashara hizo. Mwaka 2022 Wakala iliandaa zoezi maalumu la kutatua migogoro ya aina hii ili kuhakikisha kuwa biashara zinaepukana na changamoto hii.

Zoezi hili lilipewa Jina la Suluhisha na BRELA ambayo ilifanyika kuanzia Juni 13 hadi 19, 2022 ambalo ilitekelezwa kwenye kumbi zilizopo ndani ya Makumbusho ya Taifa Jijini Dar es Salaam.

UKAGUZI ELIMISHI

BRELA imekwa na utaratibu wa kuwatembelea wafanyabiashara katika maeneo yao kwa ajili ya kuweza kutambua changamoto wanazokutana nazo, kuwapa elimu ya kuhusu faida za urasimishaji biashara na kuwashamasisha kufanya sajili.

Mpaka sasa Wakala imeweza kuwatembelea na kuwafikia wamiliki wa viwanda katika Dodoma, Morogoro, Katavi, Pwani, Kilimanjaro, Kagera, Rukwa na Dar es Salaam.

Kwa dhima hiyo hiyo Wakala umefanya ukaguzi elimishi wa Leseni za Biashara Kundi "A" katika Mikoa nane (8) ya Tanzania bara ambayo ni Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Kagera Shinyanga, Tanga na Mwanza.

Na kwa Mkoo wa Dar es Salaam Makampuni 60 yamefikiwa na wahusika kupewa elimu kuhusu uwasilishaji wa Mizania ya Mwaka na faida zake ili kuwajengea uwezo wamiliki wa Kampuni faida za kutekeleza takwa hilo la kisheria na kuepuka faini za kuchelewa kuwasilisha.

KUWAJENGEA UWEZO MAAFISA BIASHARA

Kwa kutambua umuhimu wa Maafisa biashara katika kuwawezesha wamiliki wa biashara ndogo na za kati kuzilea na kuzikuza. Kwa dhima hiyo Wakala inatekeleza mpango maalumu wa kuwajengea uwezo maafisa biashara na tehama katika Mikoa yote ya Tanzania bara.

Mpaka sasa Wakala imetekeliza lengo hilo kwa kutoa mafunzo kwa Maafisa biashara wa Mikoa kumi na tisa (19) ambayo ni Tabora, Kigoma, Katavi, Shinyanga, Pwani, Dar es salaam, Lindi, Mtwara, Singida, Dodoma, Morogoro, Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Rukwa, Songwe, Lindi na Mtwara.

Jitihada hizi zinazofanywa na Wakala ni kuhakikisha kwa biashara ndogo na za kati zinalelewa na kufika pale zilipokusudiwa.



Mjasiriamali akionesha Alama ya Biashara ya bidhaa yake.

ELIMU YA URASIMISHAJI WA BIASHARA

Wakala imeweza Jitihada katika kuhakikisha kwamba Wadau wote wanapata elimu kuhusu faida na hasara ya urasimishaji wa biashara.

Katika kutekeleza hilo Wakala imekuwa ikishiriki kutoa elimu kwa wadau wake kupitiqa njia za ana kwa ana, semina, warsha, Maonesho, mafunzo na hata elimu kuititia vyombo vya Habari na mitandao ya kijamii.

Kupitia njia hizi, Wakala imeweza kuwafikia wadau wake mbalimbali na kuwashamasisha kuhusiana na faida na hasara zinazo ambatana na urasimishaji wa biashara hizo. Wadau pia wamepata fursa ya kurasimisha biashara zao papo kwa papo pale wanapokutana na maafisa wa BRELA katika shughuli mbalimbali.

KUHAMASISHA KUKUZA MITAJI

Biashara ndogo na za kati zimekuwa zikikutana na changamoto ya kuwa na mitaji midogo kwa ajili ya kuijendesha. BRELA kwa kutambua hilo imekua ikihamasisha wamiliki wa biashara hizo kuweza kuzirasimisha biashara zao ili kupata mitaji kuititia taasisi za kifedha

Kwa wamiliki wa biashara watatakiwa kusajili Jina

la Biashara, Kampuni, kuwa na cheti cha usajili wa kiwanda ili kutambulika kisheria na taasisi za fedha hasa benki kutambua uwepo wa biashara hizo kihalali na kuzipatia mitaji

KULETA USHINDANI KATIKA MASOKO

Kuna faida nyingi biashara inapokuwa imerasimishwa. Moja ya faida hizo ni kuitangaza biashara au bidhaa katika masoko ya kishindani kwa bidhaa au huduma inayotolewa au kuitangaza biashara husika ili wadau waweze kutambua ilipo na kufika kwa urahisi.

Ili kufanikisha hilo, Wafanyabiashara wamekuwa wakihamasishwa kurasimisha biashara zao na matokeo yake ni kuweza kujitangaza kwa wadau wengi zaidi na kuwafikia wadau wengi pamoja na fursa katika Nyanja tofauti tofauti.

KUHUSU HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA BRELA

Wakala inatoa huduma sita ambazo ni Usajili wa Kampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, Hataza, Kutoa Leseni za Biashara Kundi "A", Cheti cha Usajili wa Kiwanda na Leseni ya Kiwanda.

Ili mtu aweze kusajili kampuni Mwombaji anatakiwa kuwa na namba ya kitambulisho cha Taifa kutoka NIDA, Namba ya kitambulisho cha Taifa kutoka NIDA ya kila mwanahisa.

Namba ya kitambulisho cha Taifa kutoka NIDA au pasi ya kusafiria kwa raia wa kigeni na namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) ya kila mkurugenzi.

Aidha mwombaji atatakiwa kuandaa na



Wajasiriamali wakiwa katika harakati za kuuza bidhaa zao.

kuambatisha nyaraka ambazo ni Katiba ya Kampuni, Fomu ya uadilifu, Fomu ya majumuisho (Consolidated Form).

Ili kusajili Jina la biashara Mwombaji anatakiwa kuwa na namba ya kitambulisho cha Taifa kutoka NIDA, anuani ya barua pepe hai, anuani ya eneo la biashara, anuani ya makazi ya mmiliki pamoja na namba ya simu hai.

Mfanyabiashara atakayehitaji kusajili Alama ya biashara au huduma Mwombaji anatakiwa kuwa na namba ya kitambulisho cha taifa kwa raia wa Tanzania na pasi ya kusafiria kwa raia wa kigeni. Mwombaji atatakiwa kuwasilisha namba ya simu pamoja na barua pepe hai.

Nyaraka ambazo mwombaji atatakiwa kuambatisha ni pamoja na Picha au mchoro wa alama, Fomu ya majumuisho (Consolidated form) na Fomu TM/SM 1 kama mwombaji ni mwakilishi.

Kwa upande wa leseni za biashara mwombaji anaweza kutuma maombi yake kama mtu binafsi au kama Kampuni au Jina la Biashara.

Mahitaji ya kupata leseni ya Biashara kundi A kwa mtu binafsi ni pamoja na Namba ya kitambulisho cha taifa ya mwombaji wa leseni, Namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN), Uthibitisho wa sehemu ya kufanya biashara Mfano mkataba wa pango, leseni ya makazi au hati. Hati ya kuonyesha kutodaiwa kodi (Tax Clearance Certificate) na Kibali kutoka mamlaka ya udhibiti (Kutegemea na aina ya biashara).

Kwa maombi ya Leseni hiyo kwa Jina la biashara au Kampuni mwombaji anatakiwa kuwa na Hati ya usajili wa kampuni au Jina la biashara

Taarifa kutoka kwa msajili [extract from Register] kwa majina ya biashara pekee,

Namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN) ya kampuni au mwenye jina la biashara.

Hati ya kuonyesha kutodaiwa kodi (Tax Clearance Certificate) kwa anayehuisha leseni.

Uthibitisho wa sehemu ya kufanya biashara mfano mkataba wa pango, leseni ya makazi au hati ya kumiliki ardhi na Uthibitisho wa uraia na ukaazi kwa Wakurugenzi na Wanahisa wa kampuni.

Kwa upande wa Cheti cha Usajili wa Kiwanda na leseni za kiwanda mwombaji atatakiwa kandaa nyaraka za kuambatisha ambazo ni Mchanganuo wa mradi, Uthibitisho wa mahali kilipo kiwanda na Fomu ya majumuisho (consolidated form).

Izingatiwe kwamba huduma zote zinatolewa kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya BRELA www.brela.go.tz au www.business.go.tz.

Mwombaji halazimiki kufika katika ofisi za Wakala kwa ajili ya huduma hizi bali anaweza kujihudumia kwa njia ya mtandao.

Aidha Wakala pia inatoa usaidizi wa haraka kupitia kituo cha miito pale ambapo mwombaji anakua amekwama anaweza kupiga namba +255(0)222 212 800.,

BRELA yaibuka mshindi wa pili katika maonesho Morogoro

Na Pater Tweve

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeibuka mshindi wa pili kati ya taasisi 15 za Serikali zilizoshiriki kutoa huduma kwenye maonesho ya Tano (5) ya Mifuko ya Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, mkoani Morogoro.

Akizungumza mara baada ya kukabidhiwa tuzo hiyo ya ushindi wa pili na Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Dkt. Ashatu Kijiji (Mb), hivi karibuni, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa alisema, ushindi huo umetokana na huduma ambazo maafisa wa BRELA wamekuwa wakizitoa kwa wananchi wa Manispaa ya Morogoro wakati wote wa maonesho.

Bw. Nyaisa alisema wakati wote wa maonesho wananchi wamefurika kwa wingi katika banda la BRELA kupata elimu na kurasimisha biashara zao huku wengi wakikamilisha usajili wa majina ya biashara na kutoka na cheti cha usajili papo kwa papo.

"Lengo kuu la kushiriki Maonesho haya ni kutoa huduma bora na kwa muda mfupi, ili kufanikisha hilo wafanyakazi wote wamekuja na vitendea kazi vyao, hivyo mwananchi akifika banda la BRELA anapata majibu ya maswali yake yote pamoja, ushauri na huduma ya papo kwa papo" alifafanua Bw.Nyaisa.

Bw. Nyaisa aliwasihii wafanyabiashara kutumia mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao kurasimisha biashara zao kwani huduma hiyo kwa sasa ni rahisi na

inamuwezesha muombaji kupata huduma bila kufika katika ofisi za taasisi hiyo.

Aidha Bw. Nyaisa alisema kuwa mfumo uliopo sasa wa urasimishaji biashara ni rahisi na rafiki zaidi kwa waombaji wote walio mjini na vijijini, hivyo ni vyema wafanyabiashara kuacha tabia ya kuwatumia "vishoka" kurasimisha biashara zao.

"Kwa sasa mfanyabiashara siyo lazima kufika kwenye ofisi za zetu, unaweza kupata huduma ukiwa hata sebuleni kwako na ukapata cheti bila ya usumbu wowote,"alisitiza Bw. Nyaisa.

Taasisi iliyoshinda nafasi ya kwanza katika maonesho hayo ni Shirika la Posta Tanzania, huku Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ikichukua nafasi ya tatu.



Watumihi wa BRELA wakiwa na Cheti na Tuzo ya ushindi baada ya kushiriki katika maonesho ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC). Katika maonesho hayo BRELA ilipata ushindi wa pili katika utoaji huduma ikiwa ni mionganoni mwa Taasisi 15 za Serikali zilizoshiriki katika maonesho hayo Mkoani Morogoro.



A CALL FOR COMPANIES TO FILE ANNUAL RETURNS

The Registrar of Companies calls all companies incorporated and in Tanzania to file their annual returns as required by the Companies Act, CAP 212.

HOW TO FILE ANNUAL RETURNS THROUGH THE ONLINE REGISTRATION SYSTEM

1. Log in on the Online Registration System (ORS).
2. Select e - service.
3. Select Company .
4. Select Filing of annual return (accounts) / Update.
5. Fill in Incorporation/Compliance number.
6. Fill in company's details.
7. Upload form 128 together with a signed and dated consolidated form and the Financial Statement
8. Select mode of payment (Mobile or Bank).
9. After payment the application will be received for review.

Note: Filing fee of an annual return is TZS.22,000.00 if submitted on time. Delayed submission of an annual return attracts a late filing fee of TZS.2,500.00 (compounded) per every month delayed or part thereof.

DODOMA OFFICE

PSSF Building
Makole Street 10th Floor

MWANZA OFFICE

Regional Commissioner Office
Opposite TRA

"We give legal life to your business"

BRELA House, Plot No 23, Block No. 20,
Shaaban Robert Street/ Sokoine Drive, P.O Box. 9393, 11101 Ilala, Dar es Salaam.
Telephone:+ 255 22 2212800, E-mail: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz,
Website: www.brela.go.tz

A CALL FOR FOREIGN COMPANIES TO FILE FINANCIAL STATEMENT

The Registrar of Companies calls all foreign companies with registered branches in Tanzania to submit their Financial Statements as required by the Companies Act, Cap 212.

HOW TO FILE FINANCIAL STATEMENTS THROUGH THE ONLINE REGISTRATION SYSTEM

1. Log in on the Online Registration System (ORS)
2. Select e service
3. Select Company
4. Select Filling of annual return(accounts)/update
5. Fill in Compliance number
6. Fill in Company details
7. Upload audited financial statement together with consolidated form
8. Click proceed button
9. An application will be received by Business Registrations and Licensing Agency (BRELA) for review and process
10. After the review and processing of an application, an invoice will be sent to the customer for payment of the required fee.

Note: Submission of financial statement costs USD,220.00 if submitted on time. Delayed submission of financial statements are charged USD,25.00 (compounded) per every delayed month.

DODOMA OFFICE

PSSF Building
Makole Street 10th Floor

MWANZA OFFICE

Regional Commissioner OfPce
Opposite TRA

“We give legal life to your business”

BRELA House, Plot No 23, Block No. 20,
Shaaban Robert Street/ Sokoine Drive, P.O Box. 9393, 11101 Ilala, Dar es Salaam.
Telephone:+ 255 22 2212800, E-mail: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz,
Website: www.brela.go.tz

BRELA yaibuka mshindi wa pili maonesho ya Sabasaba



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA



Certificate of Award

This is to certify that

BUSINESS REGISTRATION AND LICENSING AGENCY (BRELA)

Participated in the 46th Dar es Salaam International Trade Fair
from 28th June - 13th July, 2022

and Awarded **SECOND WINNER** Prize.

Category: TRADE AND INVESTMENT PROMOTION AND FACILITATIONS EXHIBITORS



Dar es Salaam
International Trade Fair 2022



Latifa Mohamed Khamis
Director General, Tanzania Trade Development Authority



Na Nehemia Mihayo

"Niwaombe taasisi za Serikali na taasisi binafsi kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuondoa changamoto zilizopo na kufungua milango ya uwekezaji, lakini pia nanyi wafanyabiashara muwe wawazi kwa kueleza ni nani anawakwamisha ili tuyashughulikie Kwa haraka," ameongeza Dkt. Mpango.

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeibuka mshindi wa pili katika kipengele cha Uhamasishaji, Uwezeshaji Biashara na Uwekezaji, katika Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa yaliyofanyika katika viwanja vya Mwl.Julius Nyerere barabara ya kilwa Temeke, jijini Dar es salaam.

Katika maonesho hayo ya kimataifa yaliyohit mishwa tarehe 13 Julai, 2022 na Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.Philip Isdory Mpango, amelizitaka taasisi zinazowezesha biashara nchini ikiwemo BRELA kufanya kazi Kwa weledi ili kufungua milango ya uwekezaji nchini na kupunguza vikwazo kwa uwekezaji.

Katika hafla hiyo Makamu wa Rais Dkt.Mpango alizitaka taasisi zinazowezesha biashara nchini kujituma na kufungua milango ya kibiashara baina ya Tanzania na mataifa ambayo bado hayajafikiwa, ili kuongeza wigo wa

kibiashara kwa wawekezaji na Taifa kwa ujumla.

Aliongeza kuwa Wizara zinazohusika na masuala ya uwekezaji zifungue mipaka kwa kutatua changamoto zinazowakazwa wawekezaji, huku akiwataka wafanyabiashara kuwa wawazi kuelezea kinachowatatiza ili kifanyiwe kazi kwa haraka na hatimaye kuondoa vikwazo.

"Niwaombe taasisi za Serikali na taasisi binafsi kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuondoa changamoto zilizopo na kufungua milango ya uwekezaji, lakini pia nanyi wafanyabiashara muwe wawazi kwa kueleza ni nani anawakwamisha ili tuyashughulikie Kwa haraka," aliongeza Dkt. Mpango.

Pia alizitaka taasisi za Fedha kuwawezesha kiuchumi wawekezaji, ili kupata mitaji kwani janga la uviko-19 lilisababisha biashara nyinyi kuyumba.

Huduma za BRELA zamvutia Waziri



Alie kuwa Waziri wa Malialisili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akipata maelezo kutoka kwa Afisa wa BRELA, Bi Mgeni Shaban (kulia)kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala, alipotembelea banda la BRELA katika Maonesho ya Sabasaba Jijini Dar es Salaam.

Na Mwandishi wetu

WAZIRI wa Malialisili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (MB) ameipongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa utoaji wa huduma kupitia mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtando (ORS) na kuitaka taasisi hiyo kuendelea kushiriki katika maonesho ili kukuza uelewa wa wananchi juu ya matumizi ya mfumo huo.

Mhe. Balozi Chana alitoa wito huo wa BRELA moja ya mabanda ya BRELA yaliyopo katika viwanja vya Mwalimu Nyerere, barabara ya Kilwa kwenye Maonesho

ya 46 ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea jijini Dar es Salaam.

Wito huo wa Mhe. Waziri unafuatia maelezo yaliyotolewa na Afisa Huduma kwa Mteja Bi. Mgeni Shaban, baada ya Mhe. Waziri kutaka kufahamu changamoto zilizopo na kuelezwu kuwa baadhi ya wadau hushindwa kurasi mbaishara zao kutokana na kutojua kutumia mfumo huo.

"BRELA muendeleo kushiriki katika maonesho haya na mengine ikiwa ni pamoja na kuandaa warsha mbalimbali kwa wadau, juu ya matumizi ya

mfumo huu ili kukuza uelewa kwa wananchi wengi zaidi," alisitisiza Mhe. Balozi Dkt. Chana.

Alisema pia anatambua kuwa taasisi mbalimbali zinashikirikiana na BRELA ili kupata taarifa, pia kama Wizara watahimiza na kuendelea kutumia mfumo wa BRELA kupata taarifa sahihi za makampuni.

Katika Hatua nyingine Mhe. Waziri aliwapongeza wadau waliofika katika banda la BRELA ili kurasi mbaishara zao na kuwataka wakawé mabalozia na kuwahimiza wengine kufika na kupata huduma za BRELA.

Na Theresa Chilambo

Mabalozi wafurahishwa na BRELA

Mabalozi wa Zimbabwe na Malawi nchini Tanzania wamefurahishwa na kupongeza jitihada zinazofanywa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na kwa namna inavyosaidia wawekezaji wanaokuja nchini Tanzania.

Mabalozi hao, Mhe. Lt. Gen. (Rtd) Anselem Nhamo Sanyatwe, Balozi wa Zimbabwe na Mhe. Andrew Kumwenda, Balozi wa Malawi wametoa pongezi hizo baada ya kupewa taarifa namna BRELA inavyotoa huduma na kusaidia wawekezaji ndani ya Kituo cha huduma ya pamoja katika ofisi ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Bw. Abdulkarim Nzori Msaidizi wa Usajili aliwaeleza Mabalozi hao kuwa BRELA imeweka

dawati TIC ambapo kila mwekezaji anayekuja nchini anapewa huduma kwa karibu na usaidizi wa haraka ili kuanza biashara bila kikwazo chochote.

“BRELA ni lango la kila mwekezaji anayekuja nchini kufanya biashara maana atahitajika kwanza kuomba leseni za biashara”, alieleza Bw. Nzori

Naye Mhe. Balozi Lt. Gen. (Rtd) Anselem Sanyatwe alisema kuwa amefurahishwa kusikia kuwa mwekezaji yeyote nchini anapata huduma zote za BRELA ndani ya siku tatu baada ya ukamilishaji wa nyaraka zote.

Mabalozi hao walitembelea banda la BRELA kwenye Maonesho ya Mara Business Expo 2022 yaliyofanyika Musoma mkoani Mara.



Afisa wa BRELA, Bw. Abdulkarim Nzori akifanua jambo kwa Balozi Lt. Gen. (Rtd) Anselem Nhamo Sanyatwe, Balozi wa Zimbabwe na Mhe. Balozi Andrew Kumwenda, Balozi wa Malawi nchini Tanzania walipotembelea banda la BRELA katika maonesho ya MARA EXPO mkoani Mara.

BRELA yashauriwa kusaidia wafanyabiashara mkoani Mara

Aliyekuwa Rais wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA), Bw. Paul Koy ameishauri Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kusaidia wafanyabiashara wa mkoa wa Mara ili warasimishe biashara zao.

Kauli hiyo aliitoa alipotembelea banda la BRELA kwenye Maonesho ya Mara Business Expo 2022 yaliyofanyika Musoma, mkoani wa Mara

"Nawaomba sana BRELA muwasaidie wafanyabiashara wa mkoa huu maana wanahitaji sana huduma zenu", alieleza Bw. Koy

Bw. Koy alisitisiza kuwa mbali na kutoa huduma za usajili na utoaji wa leseni kwenye banda inabidi BRELA itoe elimu kwa wananchi wanaozalisha bidhaa mbalimbali.

Kwa upande wake Afisa Leseni wa BRELA, Bw. Rajab Chambega alimhakikisha kuwa Taasisi hiyo imejipanga vema kutoa huduma kwa



Aliyekuwa Rais wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA), Bw. Paul Koy (kulia), akitoa maelekezo kwa maafisa wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), alipotembelea banda la BRELA kwenye Maonesho ya Mara Business Expo 2022 yaliyofanyika Mjini Musoma, mkoani Mara.

wafanyabiashara wa mkoa wa Mara na mikoa jirani wanaotembelea maonesho hayo.

Pia alieleza kuwa kila mfanyakishaa anayeshiriki maonesho hayo atatembelewa na

kupewa ushauri na pia kusaidiwa kurasimisha biashara yake.

BRELA ilishiriki kwenye Maonesho ya Mara Business Expo 2022 na kutoa huduma za usajili na utoaji wa leseni papo kwa hapo.

UTARATIBU WA KUHUISHA TAARIFA ZA KAMPUNI

Ingia kwenye akaunti yako ya ORS kwa kutumia jina la mtumiaji na neno la siri, bofya Huduma mtandao chagua Kampuni, chagua kuwasilisha Mizania ya mwaka na hesabu kisha bonyeza endelea, ingiza namba ya kampuni kisha bofya tafta.

JAZA TAARIFA ZA KAMPUNI KAMA IFUATAVYO

1. Jina la kampuni na anwani
2. Namba za vitambulisho vya taifa vya wakurugenzi na wanahisa
3. Namba za Utambulisho wa Mlipa Kodi
4. Anwani ya makazi ya wakurugenzi na katibu wa kampuni
5. Namba za simu za wakurugenzi na wanahisa
6. Mtaji wa kampuni na mgawanyowa hisa kwa kila mwanahisa, kwa kampuni yenye mtaji
7. Katika sehemu ya viambatisho weka fomu namba 128, fomu ya majumuhisho au fomu yamabadiliko ya taarifa za kampuni

BRELA yaja na muarobaini wa migogoro katika kampuni



Kaimu Mkurugenzi wa Makampuni na Majina ya Biashara wa BRELA, Bw. Meinrad Rweyemamu akizungumza na vyombo vya habari kwenye wiki maalum ya "Suluhisha na BRELA" iliyofanyika katika Ukumbi wa Makumbusho ya Taifa, Jijini Dar es Salaam.

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inakutana na wadau wenye migogoro katika kampuni mbalimbali ili kuwezesha kampuni hizo kufanya kazi kama iliyokusudiwa katika uanzishwaji wake.

Akizingumza na vyombo vya habari kwenye wiki maalum ya "Suluhisha na BRELA" iliyofanyika katika Ukumbi wa Makumbusho ya Taifa, uliopo Mtaa wa Shaaban Robert, Jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Makampuni na Majina ya Biashara kutoka BRELA, Bw. Meinrad Rweyemamu amesema, kampuni zinaweza kuendeshwa bila migogoro endapo uendeshwaji wake

utazingatia Sheria.

Bw Rweyemamu aliwataka wamiliki wote wa kampuni ambaio wanakumbana na changamoto katika uendeshaji wa kampuni zao, kufika na kupatiwa huduma, kwani Msajili ametoa muda wa wiki moja ambapo migogoro katika kampuni itapatiwa ufumbuzi kwa kushauriana na wataalamu kutoka BRELA.

"BRELA ni mlango wa kufungua biashara hapa nchini, lakini pia ni kitovu cha uwekezaji na taarifa zote za wamiliki zipo kwetu, lakini mabadiliko yoyote yanapofanywa katika kampuni yanapaswa kuridhiwa na wahusika, vinginevyo huwa ni chanzo kimojawapo cha migogoro katika

kampuni, " alifafanua Bw. Rweyemamu.

Aliongeza kuwa wakati mwingine mwanahisa wa Kampuni, hisa zake zinaweza kutaifishwa au kutolewa kwenye umiliki wa kampuni bila ya kufuata utaratibu, hivyo katika wiki hii ya suluhisha na BRELA wote wenye changamoto za namna hiyo wafike na kupatiwa ufumbuzi.

Aidha aliwataka wale wote ambaio wazazi wao wamefariki na kudhulumiwa hisa zao au haki zao za msingi, wafike katika "Suluhisha na BRELA" yote yatafanyiwa kazi kwa mujibu wa Sheria.

"Suluhisha na BRELA" ni kampeni maalum iliyofanyika kwa lengo la kutatta migogoro kwenye kampuni ili ziwe huru kijijendesha kulingana na lengo la uanzishwaji wake.

Wakati huohuo BRELA ilipongezwa kwa kuja na wiki ya Suluhisha na BRELA, yenye lengo la kutatta migogoro mbalimbali katika kampuni.

Akizingumza baada ya kupata huduma katika Ukumbi wa Makumbusho ya Taifa uliopo mtaa wa Shaaban Robert, mkabala na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)Jijini Dar es salaam,

Bw Theophil Kimaro ambaye ni Mkurugenzi wa kampuni ya TRINE CONSULT, alisema

huduma hii imetoa mwanga kwake na amepata suluhu ya changamoto iliyokuwa ikimkibili.

Aliongeza kuwa kabla ya kufika BRELA alishindwa kipatia ufumbuzi wa haraka changamoto iliyokuwa inamkibili, lakini baada ya kufika na kuzungumza na maafisa wa BRELA suala lake limepatiwa ufumbuzi wa haraka na amepewa ushauri wa kujenga hivyo ataondokana na migogoro katika kampuni yake.

"Haikuwa rahisi kuepuksa na lilokuwa likinitatiza lakini baada ya kupata matangazo kuwa kuna Suluhisha na BRELA, nimelazimika kufika ili kupata huduma na hakika hajachukua hata zaidi ya nusu saa, tayari suala langu wamelimaliza na sasa naenda kulifanyia kazi," alifafanua Bw. Kimaro.

Bw. Kimaro aliiptaka BRELA kufanya kampeni kama hii mara kwa mara ili wadau wengi wapate fursa ya kushauriwa na kutatuliwa changamoto zao.

BRELA
Tunaiipa Uhai wa kisheria Biashara yako

BRELA wapatiwa mafunzo ya afya

Na Sheila Mfunami

TUME ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) imewataka Watumishi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kulinda afya zao pamoja na kuangalia mienendo ya maisha yao ya kila siku ili kuepuka magonjwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na msongo wa mawazo na kufanya afya ya akili kuwa imara.

Rai hiyo ilitolewa na Mtaalam wa Afya ya Akili kutoka TACAIDS. Bi. Violeth Ndosi, wakati wa mafunzo kuhusu Virusi vya UKIMWI na UKIMWI, Magonjwa Sugu yasiyoambukiza na Afya ya Akili mahala pa kazi, katika Ukumbi wa Chuo cha utalii jijini Dar es Salaam.

Bi. Ndosi alieleza kuwa karibia asilimia 50 ya msongo wa mawazo unatokea mahali pa kazi na hii ni kutokana na watumishi kutotimiza wajibu wao na kutokujali muda.

Aliongeza kuwa ni vizuri kila mmoja akawa balozi wa maisha yake katika kujali afya, kujali watu wanaomzunguka, kujali kazi na nafasi yake kazini kwani yote haya yakitimizwa yatasaidia kupunguza msongo wa mawazo na kufanya afya ya akili kuwa imara.

Bi. Ndosi alisema kuwa maisha ya sasa yamebadilika kutokana na utandawazi kwani watu wanajali sana shughuli zao na kukosa muda wa kukaa karibu na familia zao.

Alifafanua kuwa kutokana na hali hiyo malezi ya watoto yamekuwa ni changamoto na kusababisha vijana wengi kuathirika kisaikolojia kutokana na mazingira wanayoishi.

"Sasa hivi kumekuwepo na ongezeko la wavuta bangi, mashoga, wanaojiuza pamoja na vibaka jambo ambalo si jema kwa ustawi wa jamii na ndiyo chanzo kimojawapo cha maambukizi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI," alifafanua Bi. Ndosi.

Pia Bi. Ndosi aliwataka watumishi kutenga muda kwa ajili ya mazoezi pamoja na kuzingatia mlo kamili wa kila siku ili kuwa na afya bora.

Kwa upande wake Dkt. Patrick Kanyamwenge kutoka TACAIDS akiwasilisha mada kuhusu magonjwa sugu yasiyoambukiza amesema kuwa yapo magonjwa mengi sugu yasiyoambukiza ambayo yamekuwa yakiathiri mwenendo wa maisha ya kila siku, hivyo ni vyema watumishi wakitambua afya zao mapema na kuweka mipango madhubuti ya kuhakikisha Afya zao zinaendelea kuwa imara.

Dkt. Kanyamwenge alitoa ufanuzi wa aina mbalimbali ya magonjwa yasiyoambukiza yanavyoathiri watu wengi na kusababisha hata kuharibu mfumo wa maisha yao kiujumla.

Aidha Dkt. Kanyamwenge alieleza kuwa magonjwa haya yamekuwa yakiathiri sana mfumo wa maisha na kusababisha wengi kutofikia malengo pamoja na ndoto



Mtaalam wa Afya ya Akili kutoka Tume ya kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), Bi. Violeth Ndosi, alitoa mafunzo juu ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI, Magonjwa Sugu yasiyoambukiza na Afya ya Akili mahala pa kazi.

zao ambayo ni pamoja na kisukari, moyo, figo, saratani na mengine mengi.

Dkt. Kanyamwenge Aliwataka watumishi wa BRELA kupima afya zao mara kwa mara na kuzingatia mienendo ya maisha yao ya kila siku, ili kukabiliana na magonjwa yasiyoambukizwa.

Akifunga mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Huduma na Uwezesaji Bw. Daimon Kisyonbe alimshukuru Dkt. Kanyamwenge pamoja na Bi. Ndosi kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA kwa kuthamini afya za watumishi kwa kuwapatia elimu juu ya VVU, UKIMWI, magonjwa sugu yasiyoambukiza na Afya ya Akili mahala pa kazi.

Wakandarasi watakiwa kutoa ushirikiano kwa BRELA

Na Njwaba Mwijibie

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imewataka wakandarasi nchini kuendelea kutoa ushirikiano kwa BRELA ili kuwezesha kazi zao kufanyika kwa ufanisi zaidi

Hayo yilibainishwa na Afisa Usajili wa BRELA, Bw. Gabriel Girangay wakati wa mkutano wa wakandarasi katika ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Bw. Girangay alisema, Wakandarasi ni wadau muhimu hivyo wanapaswa kutoa ushirikiano wa karibu kwani kabla ya kwenda kusajiliwa na Bodii ya Usajili wa Wakandarasi wanatakiwa kusajili kwanza makampuni yao BRELA.

"Wakandarasi ni watu muhimu na inapaswa kuhakikisha mnahuisha taarifa zenu kwa wakati ili muweze kutambulika kwenye mfumo na iwasaidie kushindana katika zabuni mbalimbali zinazotangazwa." amesema Bw. Girangay

Aliongeza kuwa, wakati wa kuhuisha taarifa za wanahisa BRELA ni kiungo muhimu hivyo ni vyema kutoa ushirikiano wa kina ili kufanikisha shughuli zao za ukandarasi.

Pia aliwasihii kuacha kuwatumia "vishoka" ambao wanababishi ucheleweshaji wa michakato wa urasimishaji wa biashara.

Alieleza kuwa, mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtando (Online Registration System-ORS) unatoa nafasi kwa kampuni kupata huduma za BRELA mahali popote.



Afisa Usajili wa BRELA, Bw. Gabriel Girangay akitoa elimu.



Waziri wa ujenzi Prof. Makame Mbarawa (Mb), akimkabidhi cheti cha ushiriki Afisa Usajili wa BRELA, Bw. Gabriel Girangay, wakati wa mkutano wa wakandarasi katika ukumbi wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

BRELA yatoa msaada kwa yatima

Na Nehemia Mihayo

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imetua mahitaji katika Kituo cha Watoto Yatima Mwandalishi, kilichopo Mbweni Jijini Dar es Salaam.

Baadhi ya mahitaji yaliyotolewa ni pamoja na mafuta ya kupikia, sabuni, unga wa sembe, mchele, maharage, madaftari, nguo, dawa ya meno, penseli na kalamu.

Mkurugenzi wa Huduma na Uwezesaji kutoka BRELA, Bw. Daimon Kisyombe alieleza kuwa lengo kubwa ni kuwatia moyo watoto hao ili kuongeza juhudhi ya kuzifua ndoto zao.

"BRELA ni taasisi ambayo inasimamia urasimishaji wa biashara, kwa miaka ijayo watoto hawa ndio tunatarajia washike hatamu katika uanzishwaji wa viwanda, ubunifu na biashara mbalimbali," amefafanua Bw. Kisyombe.

Bw Kisyombe aliongeza kwa kusema kuwa mbegu inayopandwa ndani ya vijana hawa siku ya leo, inatarajiwa kuzaa matunda ambayo yatawanufaisha wao, jamii na taifa kwa ujumla.

Nae, Bi. Roida Andusamile ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano kutoka BRELA, alieleza kuwa katika kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma Taasisi itakutana pia na wadau wengine.

"Kuwashika mkono watoto hawa



Mkurugenzi wa Huduma na Uwezesaji kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Daimon Kisyombe akimkabidhi Katibu wa Kituo cha Watoto Yatima Mwandalishi, Bw. Omari Abdul Madaftai kwa ajili ya Watoto wanaolelewa katika kituo hicho kilichopo Mbweni Jijini Dar es Salaam.

ni moja ya shughuli zitakazofanyika katika wiki hii, shughu

li nyngine ni pamoja na huduma za papo kwa papo katika ofisi zetu zilizopo kwenye makutano ya Mtaa wa Shaaban Robert na barabara ya Sokoine, jijini Dar es Salaam,

Katibu wa Kituo cha Watoto Yatima Mwandalishi, Bw. Omari Abdul alisema kuwa ujio wa BRELA kituoni hapo ni faraja kwao kama

walezi wa watoto hao. Pia walipata fursa ya kujifunza kazi zinazofanywa na taasisi hiyo, elimu ambayo itakuwa na manufaa makubwa kwoo.

Mtoto Husna Issa anayelelewa katika kituo hicho, alishukuru uongozi wa BRELA kwa kuwafikia na kuwapa usaidizi. Pia alitoa wito kwa taasisi binafsi na za umma kuwashika mkono ili waweze kuzifikia ndoto zao.



Baadhi ya Watumishi wa BRELA, wakiwa katika picha ya pamoja na Watoto wanaolelewa katika Kituo cha Watoto Yatima Mwandalishi kilichopo Mbweni, jijini Dar es Salaam.

BRELA yawafikia Wabunifu wa Vyuoni

Na Peter Tweve

Wabunifu kwenye Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya katika wameaswa kuzisajili kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bunifu zao ili waweze kuzilinda kisheria na kupata manufaa kutokana na jitihada zao.

Hayo yalisemwa Jijini Arusha hivikaribuni na Afisa Mwandamizi Utumishi na Utawala kutoka Idara ya Miliki Ubunifu (BRELA), Bw. Raphael Mtalima katika warsha ya kuwajengea uwezo watumishi na watafiti kutoka Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST).

Bw. Mtalima Alisema kuwa Wabunifu na Wavumbuzi wengi hawajui taratibu za kulinda kazi zao ili ziweze kuwafaidisha kwa kuwa wamewekeza nguvu nyingi na rasilimali katika kufanya tafiti mbalimbali mpaka kufikia hatua hiyo.

Alibainisha kuwa Sheria ya kulinda vumbuzi na bunifu mbalimbali ipo na BRELA imekusudia kutoa elimu juu ya taratibu za kusajili katika vyuo ya sayansi vilivyopo Jijini Arusha

"Lengo kuu la warsha hii ni kuwajengea uwezo wabunifu wajue umuhimu wa kuendelea na tafiti zao na kuzisajili BRELA kwaajili ya kunufaika nazo hapo badaye" alisema Bw. Mtalima.

Katika zoezi hilo Jijini Arusha, Maafisa wa BRELA walitoa elimu hiyo pia katika Chuo cha Ufundu Arusha (ATC) na Chuo Kikuu cha Makumira.

Naye Mkuu wa Idara ya Utafiti na Ubunifu katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Bi. Edna Makule alisema taasisi hiyo imefanya tafiti na bunifu mbalimbali zilizofikia hatua ya kulindwa, hiyo elimu hiyo inamamufaa kwao na watapiga hatua zaidi katika ulinzi wa bunifu zao.

Naye mmoja kati ya mwanafunzi anayesoma Shahada ya Uzamivu (PhD), Bw. Isack Kandola alisema amejifunza mambo mengi kupitia BRELA na atatunza bunifu zake ili zisiibiwe na watu wengine kutoka nje ya nchi na kusisitiza wabunifu kutunza mawazo yao kupitia taasisi hiyo.

Wakati huohuo Afisa Sheria wa BRELA Ubunifu Bw. George

Msaki akiwa katika chuo Chuo Cha Don Bosco jijini humo ali-wataka wabunifu kusajili Bunifu zao BRELA ili kuona matunda ya kazi zao.


Alisema imefika wakati kila mbunifu aone matunda ya anachokifanya kwa kujisajili BRELA.

Alisema ana imani kuwa elimu ya Miliki Ubunifu wanayoitoa vyuoni italeta chachu kwa watalam kuendelea kuvumbua na kumiliki kisheria bunifu zao kwa ajili ya maendeleo binafsi na Taifa kwa ujumla.

"Vumbuzi nyingi zipo vyuoni ndiyo maana tukaanzia huku kutoa elimu hii, tunaamini mmeleewa na matokeo yataonekana kupitia ongezeko la usajili," alisema Bw. Msaki

Aliwasihii pia wanafunzi hao kurasi mishaa biashara zao kupitia Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao unaojulikana kama Online Registration System (ORS).

Bw. Msaki alisema zoezi la utoaji elimu ya Miliki Ubunifu ni endelevu na litafanyika nchi nzima.



Wanafunzi wa Chuo Cha Don Bosco Jijini Arusha, wakiwa katika kazi ya Ubunifu, walipotembelewa na BRELA, kwa lengo la kupatiwa mafunzo juu ya umuhimu wa kusajili na kulinda vumbuzi zao.

Wahariri watakiwa kusaidia ukuaji biashara



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah akitoa hotuba katika kikao kazi cha wahariri wa vyombo vya habari na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kilichofanyika mkoani Morogoro.

WIZARA ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara imewataka Wahariri wa Vyombo vya Habari nchini kufanikisha ukuaji wa sekta ya biashara nchini.

Hayo yalismwa na Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe Dkt. Ashatu Kijiji kuptitia hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Hashil Abdallah (sasa Katibu Mkuu) katika kikao kazi cha siku mbili kati ya wahariri wa vyombo vya habari na BRELA kilichofanyika mkoani Morogoro.

"Hivyo kwa muktadha huu niwaombe wahariri tushirikiane kwa pamoja kwenye kufanikisha ukuaji wa sekta ya biashara nchini, hasa wananchi warasimishe biashara zao. Kuptitia nyie watakuwa na uelewa wa mambo mengi," alisema Dkt. Abdalah.

Pia alisema, kuptitia kikao kazi hicho anaamini wahariri watakuwa mabalozi wazuri wa BRELA kwa kuwa ajenda za wakala huo hususani kwenye urasimishaji wa biashara watazibeba ili wananchi waweze kupata taarifa njema ambazo zitawawezesha kunufaika kuptitia wakala huo.

Katika hatua nyingine, Dkt. Abdalah alisema, BRELA wanapaswa kuendelea kuimarisha ushirikiano na vyombo vyote vya habari na kila wanapotakiwa kutoa ufanuzi wa jambo fulani wasisite kufanya hivyo.

"BRELA, muelewe kuwa wahariri wana jukumu la kuandika habari kwa usawa, pindi wanapotaka kutoa habari kwenu msiwe wagumu kutoa taarifa, kama majibu ya maswali yao yapo kwa muda huo wapewe ili umma upate taarifa kwa haraka na kama habari wanayohitaji inachukua muda kupata majibu wapewe mrejesho mapema ili waweze kusubiri ili upotoshaji usiwepo.

"Mkumbuke kuwa, Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kila mtu:[a] ana

uhuru wa kuwa na maoni na kujielekeza na kutoa maoni au mawazo yake, [b] ana haki ya kutafuta, kupokea na, au kusambaza taarifa bila kujali mipaka ya nchi,

"[c] ana uhuru wa kuwasiliana na haki ya kulindwa dhidi ya kuingiliwa kati ya mawasiliano yake, na [d] ana haki ya kupata taarifa wakatin wote kuhusu matukio mbalimbali yanayoendelea kuhusu maisha. Hivyo (BRELA), mtambue kuwa ibara hii inawalinda wahariri wa vyombo vya habari katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kutoa habari muhimu zenye maslahi kwa umma na umma pia una haki ya kupata taarifa," alisema Dkt. Abdalah.

Wakati huo huo, Dkt. Abdalah alisema wahariri wanapotekeleza majukumu yao kutumia lugha rahisi kuwaeleza wananchi masuala ya BRELA, kwani mambo mengi ya wakala huo yapo kisheria.

"Wapo wahariri wengine wanawea kuwa na mitazamo tofauti kwa namna wanavyotafsiri sheria za utekelezaji wa majukumu ya BRELA na kupelekeea muda mwininge kuandika kichwa cha habari kinachopiga kelele au kichwa cha habari kinachohukumu na kuleta tarariki kwa umma, ninaamini kuptitia mkutano huu mtajadili kwa kina yale ambayo yamekuwa yakiwatatiza na kupata majibu ya kina," alisema Dkt. Abdalah.

Awali, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa alisema kuwa, usimamiaji wa majukumu ya msingi ya BRELA umewezesha kuwa na mafanikio makubwa yenye uwazi na ukuaji wa uchumi wa Tanzania.

Bw. Nyaisa alisema kuwa, hali hiyo inatokana na uboreshaji wa mazingira ya biashara na urahisishaji wa sajili na leeni zinazotolewa na BRELA hapa nchini.

"Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wa mikakati mkuu ya Kitaifa, Sera na Mpango wa Maendeleo ya Taifa," alisema Bw. Nyaisa.

MATUKIO KATIKA PICHA



Rais Mstaafu wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt.Jakaya Mrisho Kikwete, akimkabidhi tuzo ya Udhamini wa Maonesho ya Tatu ya Uwezeshaji na Biashara, Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Makampuni kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bi Leticia Zavu yaliyofanyika Mjini Kibaha Mkoa wa Pwani.



Watumishi wa BRELA, wakiwa katika picha ya pamoja waliposhiriki katika Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) jijini Dar es salaam.



FAHAMU KUHUSU MFUMO WA KUWASILISHA TAARIFA ZA WAMILIKI WANUFAIKA

Mfumo wa kupokea taarifa za Wamiliki Wanufaika ni mfumo unaojitegemea kutoka kwenye mfumo wa Online Registration System (ORS) hivyo kampuni ambazo zina maombi yanayoendelea kwenye ORS bado zinaweza kuwasilisha taarifa zake za Wamiliki Wanufaika kupitia link ya <https://bo.brela.go.tz>

.....
“TUNAIPA UHAI WA KISHERIA BIASHARA YAKO”

*152*00#

Chagua 9
Kisha 2

Pakua
eMrejesho
Mobile App



Ingia katika
Google play

Tafuta emalalamiko

Jengo la BRELA, Kitalu Na 20, Nyumba Na 23,
Barabara ya Sokoine / Mtaa wa Shaban Robert , S.L.P. 9393,
11101, Dar es Salaam. Simu: +255-22 2212800,
barua pepe: maoni@brela.go.tz, malalamiko@brela.go.tz
usajili@brela.go.tz

Tovuti: www.brela.go.tz